


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

---

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,  
ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA  
YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (FUNGU 14, 28, 29, 51 NA 93) KWA  
MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2022/2023

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu  
za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

Mei , 2022

# YALIYOMO

<b>ORODHA YA MAJEDWALI .....</b>	<b>i</b>
<b>ORODHA YA GRAFU .....</b>	<b>ii</b>
<b>ORODHA YA CHATI .....</b>	<b>iii</b>
<b>1.0 UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
<b>2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO .....</b>	<b>2</b>
2.1 Maelezo Kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa.....	3
2.2 Matokeo ya Ukaguzi.....	4
2.2.1 Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.....	4
2.2.2 Fungu 28 – Jeshi la Polisi.....	8
2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Miradi ya Maendeleo .....	9
<b>3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022... 11</b>	
3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; .....	11
3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 .....	11
3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina.....	17
3.3 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati .....	20
<b>4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 .....</b>	<b>22</b>
4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 .....	22
4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2022/2023 .....	23
4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi.....	27
<b>5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI.....</b>	<b>31</b>
5.1 Maoni ya Kamati.....	31
5.2 Ushauri wa Jumla .....	32
5.3 Ushauri Mahsus.....	32
5.3.1 Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.....	32
5.3.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi.....	34
5.3.3 Fungu 29- Jeshi la Magereza .....	34
5.3.4 Fungu 51- Wizara.....	35
5.3.5 Fungu 93 - Uhamiaji .....	36
<b>6.0 HITIMISHO.....</b>	<b>38</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

<b>Jedwali Na. 1:</b> Mwenendo wa Makusanyo ya Wizara 2017/2018 – 2021/2022 .....	13
<b>Jedwali Na. 2:</b> Mchanganuo wa Mapato hadi kufikia Februari 2022	14
<b>Jedwali Na. 3:</b> Mchanganuo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 kwa matumizi ya Wizara.....	19
<b>Jedwali Na. 4:</b> Makadirio ya Mapato .....	24

## ORODHA YA GRAFU

<b>Grafu Na. 1:</b> Mwenendo wa Makusanyo ya Wizara 2017/2018 - 2021/2022 .....	13
<b>Grafu Na. 2:</b> Ulinganisho wa Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na 2021/2022 .....	14
<b>Grafu Na. 3:</b> Mchanganuo wa upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2021/2022 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara .....	19
<b>Grafu Na. 4 :</b> Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo 2021/2022- 2022/2023 .....	26

## ORODHA YA CHATI

<b>Chati Na. 1:</b> Mgawanyo wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 .....	28
--	----

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,  
ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA  
YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (FUNGU 14, 28, 29, 51 NA 93) KWA  
MWAKA WA FEDHA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA  
HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kuliomba Bunge liipokee taarifa hii, kuikubali na, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako kuwa, uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya

Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda (*scope*) ya Taarifa hii, nalikumbusha Bunge lako tukufu kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajumuisha Mafungu matano (5) ya kibajeti yafuatayo:-

- (a) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
- (b) Fungu 28 - Jeshi la Polisi;
- (c) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;
- (d) Fungu 51 - Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA; na
- (e) Fungu 93 - Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne (4) zifuatazo:-

- (a) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- (b) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (c) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
- (d) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo mitatu (3) inayotekelezwa na Wizara hii katika Mkoa wa Dar es Salaam. Katika ziara hiyo, Kamati pia ilifuatilia na kukagua *Fire Hydrants* katika Mkoa wa Kizimamoto Ilala.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ya Taarifa inaeleza mambo makuu mawili ambayo ni:

- (a) Muhtasari wa maelezo ya Miradi iliyotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- (b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha lilizoidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

## **2.1 Maelezo Kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara hii ilipaswa kutekeleza jumla ya miradi 15 katika Mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa madhumuni ya masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi mitatu inayotekelezwa katika mkoa wa Dar es salaam. Naomba kueleza kwa muhtasari kuhusu miradi hiyo kama ifuatavyo:-

### **(a) Umaliziaji wa Jengo la Zimamoto na Uokoaji Temeke -Mchicha**

Mradi huu unahusu umaliziaji wa Jengo la Ofisi za Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dar es salaam, Temeke - Mchicha. Mradi huu unatekelezwa chini ya Fungu 14 -Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

### **(b) Ukarabati wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala**

Mradi huu unahusu kukarabati Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala na unatekelezwa chini Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.



(c) **Ukarabati wa Hanga la Kuhifadhia Ndege za Jeshi la Polisi – Dar es Salaam.**

Mradi huu unahusu ukarabati wa Hanga la Kuhifadhia Ndege za Jeshi la Polisi lililopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Mradi huu unatekelezwa chini ya Fungu 28- Jeshi la Polisi.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wake kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

(a) **Mradi wa Kumalizia Ujenzi wa Jengo la Ghorofa Tatu la Ofisi kwa Mkoa wa Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 06 Julai, 2021 kwa kutumia utaratibu wa *force accounts*. Wakati wa ukaguzi, Kamati ilielezwa kuwa ujenzi wa mradi huu unagharimu **Shilingi 2,397,178,675.40** hadi kukamilika kwake. Mwezi Juni, 2021 Serikali iliipatia Fungu 14 kiasi chote cha fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Kamati ilipotembelea na kuukagua mradi huu, ilijulishwa kuwa utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 86**.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi Kamati ilibaini kuwa mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

- (i) Eneo ambalo mradi huu unatekelezwa linamilikiwa na TAZARA;
- (ii) Licha ya mradi huu kutekelezwa chini ya utaratibu wa *force account* na fedha kutolewa tangu Mwezi Julai, 2021, miezi 9 ya kipindi cha utekelezaji, mradi umefikia **asilimia 86**. Hali hiyo inaoensha kasi ndogo ya utekelezaji ikilinganishwa na nia ya kupatiwa fedha yote mapema; na
- (iii) Uwepo wa vituo 3 vya zimamoto katika Jiji la Dar es Salaam wakati mahitaji ni vituo 13.

(b) **Ukarabati wa Jengo la Zimamoto na Uokoaji Ilala**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi 273,746,089.00** kwa ajili ya mradi huu. Hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2022 Kamati ilipotembelea mradi huu, ukarabati haukuwa umeanza. Udadisi wa Kamati ulibainisha kuwa Mradi huu haukupokea fedha iliyotengwa kutokana na kutokamilishwa kwa taratibu zilizohitajika, ikiwemo taratibu za ununuzi wa umma.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kutoanza kwa utekelezaji wa mradi huu zipo changamoto ambazo zilielezwa kuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Zimamoto na Uokoaji Ilala kama ifuatavyo:-

- (i) Kutokuwa na Hati ya Kiwanja ambacho Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Ilala zipo;
- (ii) Ukosefu na uchakavu wa magari ya kuzimia moto ambapo, ilielezwa kwamba, Kituo kina magari 13. Kati ya hayo 10 ni mabovu na hayafanyi kazi. Hali hiyo inaathiri uwezo uliokuwepo kwa magari kiasi cha asilimia 76.9 na kuacha uwezo wa magari 3 tu yanayofanya kazi.
- (iii) Uhaba wa vitendea kazi kama boti, tochi zinazotumika katika uokozi majini, maboya ya *Divers/Swimmers* na mitungi ya gesi kwa *divers*;
- (iv) Uhaba wa wataalamu wa uokozi majini (*divers* na *swimmers*). Mathalani, ilielezwa kuwa mbali ya nchi yetu kuzungukwa na Mito, Maziwa na Bahari ina *Divers* 16 tu; na
- (v) Askari kukosa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu shughuli za ukoaji hasa majini.

**(c) Ukaguzi wa Visima vya Kuchukulia Maji (*Fire Hydrant*) Mkoa wa Zimamoto Ilala**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua visima vya kuchukulia maji katika Mkoa wa Kizimamoto Ilala. Kamati ilielezwa kuwa Mkoa huo una visima vya

kuchukulia maji vinavyotambulika na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji takribani 41; ambapo 9 ni vibovu, 9 vina fanya kazi vizuri, 4 vina presha ndogo, 2 havina maji kutokana na mfumo wa maji kufungwa, 4 havifunguki kutokana na uchakavu wa miundombinu yake na 13 vimefukiwa na udongo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika ziara hiyo, Kamati ilielezwa kuwa visima vya kuchukulia maji ni muhimu sana katika Miji kwani ndivyo hutumika kujaza maji magari ya zimamoto kwa ajili ya kuzima moto pale inapotokea.

Hivyo, kutokana na ukweli kuwa kukua kwa miji kunaambatana na vihatarishi vingi ikiwemo majanga ya moto bado idadi hiyo ya visima 41 ni ndogo ukilinganisha na ukubwa wa Ilala.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi huo, Kamati ilielezwa kuwa mfumo visima vya kuchukulia maji katika Mkoa wa kizimamoto wa Ilala unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (i) Uchache wa Fire Hydrant;
- (ii) Fire Hydrants kukosa alama za utambuzi;
- (iii) Fire Hydrant kufukiwa kutokana na shughuli za kibinadamu;
- (iv) Fire Hydrant kiuendeshaji zipo chini ya Mamlaka za maji na hivyo jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni mtumiaji tu asiyeweza kufanya hata ukarabati wa miundombinu hiyo;

- (v) Wananchi kuingilia miundombinu ya Fire Hydrant kwa kujenga makazi au kuendesha biashara karibu na fire Hydrants; na
- (vi) Kutofanya ukarabati wa Fire Hydrants kwa muda mrefu na hivyo kusababisha baadhi kuharibika.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kuwa na Fire Hydrants ni kutoa huduma ya maji kwa magari ya zimamoto na pale kunapokuwa na uhitaji wa maji kwa dharura. Ilala ni Mji wa kibiashara, ikiwa Ilala ina visima vichache namna hiyo, huenda miji mingine ina visima vichache zaidi ya Ilala. Hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba, hatua stahiki za Serikali ikiwemo kuandaa mkakati wa kujenga miundombinu ya visima vingi zaidi katika miji inayokuwa nchini zinahitajika ili kuweka mazingira sawa ya kukabiliana na matukio ya moto.

### 2.2.2 Fungu 28 – Jeshi la Polisi

**Mheshimiwa Spika**, Fungu hili lilitengewa **Shilingi 271,282,318.15** kwa ajili ya Ukarabati wa Hanga la Ndege lililopo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Wakati Kamati inakagua mradi huu 16 Machi, 2022 ilielezwa kuwa tangu Mwezi Desemba, 2021 Serikali ilishatoa fedha kiasi cha Shilingi **220,000,000.00** sawa na asilimia 81.1. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa kuwa, pamoja na Serikali kutoa fedha, ukarabati wa Hanga hilo haukuwa umeanza bali ulikuwa katika hatua ya ununuzi.

**Mheshimiwa Spika**, Udadisi wa Kamati ulidhihirisha kuwa kuchelewa kuanza kwa mradi huo ni kutokana na sababu mbalimbali kama vile, kuchelewa kutolewa kwa kibali cha kutumia fedha hizo kutoka Wizarani, kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa kuunda Kamati ya Ujenzi pamoja na kuchelewa kujibiwa maombi ya vibali vya kuanza ununuzi. Vibali hivyo vilipaswa kutolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lianze hatua zinazohitajika.

### 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

- (a) Serikali kuzingatia umuhimu wa mradi wa kumaliza ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dar es Salaam kwa kutoa kiasi cha **Shilingi 2,379,178,675.40** ni jambo linastahili pongezi. Sababu ni kuwa kukamilika kwa ujenzi wa kituo hiki ni sehemu muhimu ya kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji katika jiji la Dar es Salaam. Pamoja na hivyo, uzingatiaji wa thamani halisi ya matumizi katika utekelezaaji wa mradi ni jambo la kusisitizwa na kupewa uzito stahiki.
- (b) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kushindwa kukamilisha michakato mbalimbali, ikiwemo ya ununuzi kwa kipindi cha zaidi ya miezi 9 tangu kuanza kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni dosari katika utekelezaji wa miradi. Hali hiyo inahitaji hatua za

Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi ili kurekebisha dosari hiyo kabla ya kuanza Mwaka wa Fedha 2022/2023.

- (c) Kuchakaa na kuvuja kwa Hanga la Ndege la Jeshi la Polisi ni hali inayosababisha hasara kubwa kutokana na maji kuharibu baadhi ya vipuri vinavyohifadhiwa. Kwa msingi huo, kutokutolewa kwa kibali cha Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kwa ajili ya kuanza ukarabati ni jambo linaloendeleza uwezekano wa hasara hiyo, hivyo linahitaji kurekebisha.

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa Kamati ulibaini kwamba katika Wizara ya Mambo ya Ndani; Fungu 28 limepata **zaidi ya asilimia 90** ya fedha za maendeleo kutokana na kukamilisha taratibu za kuomba fedha Hazina. Wizara hii hii, Fungu 14 hadi kufikia Machi, 2022 lilikuwa halijaanza hata michakato ya ndani kuweza kuomba fedha Hazina.

Hii inaonesha kuwa hakuna ufuatiliaji mzuri wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na fedha zinazotolewa katika Wizara hii.

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

#### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ilizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu yote Matano ya Wizara. Vilevile, Kamati ilizingatia taarifa muhimu na za ziada zilizopatikana kupitia mahojiano wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

##### **3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ikijumuisha Mafungu yake yote matano ilikadiriwa kukusanya mapato ya **Shilingi 331,591,585,600** ikilinganishwa na **shilingi 488,569,880,319/=** zilizokadiriwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari 2022, kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni **Shilingi bilioni 175.04 sawa na asilimia 52.8 ya lengo la mwaka lililopangwa**. Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yameongezeka kwa **asilimia 16.9** ikilinganishwa na



makusanyo yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa **Shilingi Bilioni 149.65 sawa na asilimia 30.63** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa kina, Kamati ilibaini kuwa Mafungu yote matano ya Wizara yalikusanya mapato kwa kiwango cha kuridhisha ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hiki kwa kila Fungu katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano na kufanya ulinganisho wa Makusanyo hayo kwa miaka mitano kuanzia Mwaka 2017/2018. Kamati ilibaini kuwa makusanyo ya Mapato yamekuwa yakiongezeka kila Mwaka hadi Mwaka 2019/2020 na kupungua katika Mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi, uchakavu wa vitendea kazi, uhaba wa rasilimaliwatu na UVIKO – 19 ni kati ya sababu zilizochangia makusanyo hayo kupungua.

Mwenendo huo wa Makusanyo unadhihirika katika Jedwali Na. 1& 2 na Grafu Namba 1 hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Wizara 2017/2018  
- 2021/2022**

MWAKA	2017/2018	2018/2019	2019/2020	2020/2021	2021/2022
MAKUSANYO	160.69	185.53	229.81	149.65	175.05


**Grafu Na. 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Wizara 2017/2018 -  
2021/2022**



**Chanzo: Randama za Wizara 2017/2018 - 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na kuainisha mchanganuo wa makusanyo kwa kila Fungu hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ikilinganishwa na lengo la Mwaka lilowekwa. Aidha, Kamati ilifanya ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana hadi kufikia Mwezi Februari 2022 na Makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho, Mwaka 2021 kama inavyoonekana katika **Grafu Na. 2** na **Jedwali Na. 2** hapa chini.

**Grafu Na. 2: Ulinganisho wa Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha  
2020/2021 na 2021/2022**



**Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021 na 2021/2022**

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Mapato hadi kufikia Februari 2022**

FUNGU	MAKADIRIO 2021/2022	% YA JUMLA YA LENGO	MAKUSANYO FEB 2022	% YA JUMLA YA MAKUSA NYO
14 – Zimamoto	9,250,000,000	2.79	5,510,850,000	3.15
28 – Polisi	90,000,000,000	27.14	41,199,422,098.41	23.54
29 – Magereza	2,000,000,000	0.60	1,709,054,439.32	0.98
51- Wizara	226,606,600	0.07	322,595,159	0.18
93- Uhamiaji	230,114,979,000	69.4	126,306,548,979.41	72.16
<b>JUMLA</b>	<b>331,591,585,600</b>		<b>175,048,470,676.14</b>	

**Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- (a) **Makusanyo ya Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto**, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 2.79** lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 14 limechangia kwa **asilimia 3.15** ya kiasi kilichokusanywa;
- (b) **Makusanyo ya Fungu 28 - Jeshi la Polisi**, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 27.14** na Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 28 limeshachangia kwa **asilimia 23.54** ya kiasi kilichokusanywa;
- (c) **Makusanyo ya Fungu 29 - Jeshi la Magereza**, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.60** na Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 0.98** ya kiasi kilichokusanywa;
- (d) **Makusanyo ya Fungu 51 - Wizara**, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.07** na Taarifa ya Makusanyo ilionesha Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 0.18** ya kiasi kilichokusanywa;
- (e) **Makusanyo ya Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji**, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 69.40** lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limeshachangia **asilimia 72.16** ya kiasi kilichokusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila Fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa Jeshi la Uhamiaji ndio iliyochangia kwa asilimia kubwa katika makusanyo yote ya Wizara. Hadi mwezi Februari, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya **asilimia 52.8** ya lengo; ingawa kwa kipindi hicho angalau wangukuwa wamefikia **asilimia 65** ya lengo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kutofikiwa kwa lengo la makusanyo kumechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi, uchakavu wa vitendea kazi, uhaba wa rasilimaliwatu na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO – 19 hali iliyopelekea kupungua kwa uingiaji na utokaji wa wageni na raia ni kati ya sababu zilizochangia kutofikiwa kwa lengo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Mwaka huu wa fedha si wa kuridhisha kwani kiujumla Wizara kwa mafungu yote imekusanya **asilimia 52.8**. Aidha, Fungu 93 limefikia lengo lake kwa asilimia 54.89 na Fungu 28 kwa asilimia 45.78. kwa mwenendo huu si rahisi kufikia lengo la makusanyo kwa mafungu haya mawili katika kipindi kilichobaki kumaliza mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mwenendo wa makusanyo ya Mapato kwa Mwaka huu kutokuwa wa kuridhisha ni dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kutokufikiwa kwa lengo lilowekwa.

Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itazingatia changamoto zilizoinishwa katika taarifa hii na

kupanga makadirio ya makusanyo kwa kuzingatia uhalisia katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### 3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya matumizi ya Wizara hususan fedha za maendeleo umendelea kuwa changamoto ya muda mrefu.


**Mheshimiwa Spika**, Katika Bunge la Kumi na Mbili Kamati iliendelea kuishauri Serikali kupitia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo utengwaji wa fedha za maendeleo na mtiririko wa upatikanaji wa fedha hizo uliendelea kuwa si wa kuridhisha kwa baadhi ya Mafungu hasa Fungu 29 na 14 na hivyo kuathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan inayohusu ukarabati wa Jengo la Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Ilala, ukarabati wa Magereza Makuu na uboreshaji wa mashamba na viwanda vya Magereza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia changamoto hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022. Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

- (a) Hadi kufikia Mwezi Februari 2022, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 62.14** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.
- (b) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2022, **asilimia 40.56** ilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo, **asilimia 58** ilikuwa ni mishahara na **asilimia 1.44** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.
- (c) Hadi kufikia Mwezi Februari 2022, Asilimia ya fedha za maendeleo zilizotolewa kwa kila Fungu ilikuwa: Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji - **asilimia 0**; Fungu 28 - Jeshi la Polisi - **asilimia 92.5**; Fungu 29 - Jeshi la Magereza - **asilimia 0**; Fungu 51- Wizara - **asilimia 46.8** na Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji lilipokea **asilimia 45.92**;
- (d) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, Mafungu mawili, 14 Jeshi la Zimamoto na 29- Jeshi la Magereza hayakuwa yamepokea fedha za maendeleo; na
- (e) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, ni fungu 28 tu lilolopokea fedha za maendeleo zaidi ya **asilimia 50**; na Fungu 51 na 93 yamepokea fedha za maendeleo chini ya asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za Mishahara, Matumizi Mengineyo na Maendeleo, umeoneshwa dhahiri katika **Grafu Na. 3** na **Jedwali Na. 3** hapa chini.

**Grafu Na. 3: Mchanganuo wa upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2021/2022 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara**



*Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022*

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 kwa matumizi ya Wizara**

Matumizi	Fedha iliyotengwa	Fedha iliyopokelewa hadi Februari, 2022	Asilimia
Mengineyo	391,886,209,021	237,202,801,315.50	60.53
Mishahara	521,868,751,000	339,217,610,621.58	65
Maendeleo	27,110,000,000	8,435,825,087.36	31.12



**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni wa kuridhisha kwani imepokea zaidi ya asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mishahara na mengineyo. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mtiririko wake sio wa kuridhisha kwani Fungu 51 na 93 yamepata fedha za maendeleo chini ya asilimia 50; na Fungu 14 Jeshi la Zimamoto na Fungu 29- Jeshi la Magereza hayakupata fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Ili idhini ya Bunge kwa bajeti ya kugharimia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iwe na tija, upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati na kwa kadiri inavyostahili, ni jambo muhimu kufanikisha utekelezaji huo kwa muda uliopangwa. Hivyo, ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha hizo kwa Mafungu yote kwa ukamilifu kufikia tarehe 30 Juni, 2022 ili kutoathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

### **3.3 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa, taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Mfano wa ushauri wa kamati uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa watumishi katika Idara na Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Taarifa iliyowasilishwa ilieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali imetoa kibali cha ajira kwa Majeshi hayo; ambapo Fungu 14 limeajiri Askari wapya 400, Fungu 28 Askari wapya 4103, Fungu 29 Askari wapya 700 na Fungu 93 Askari wapya 820.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kwa mafungu yote ili kutekeleza kwa ufanisi miradi inayopangwa. Taarifa ya Wizara ilieleza kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Fungu 51 na 93 yalikuwa yamepokea fedha za maendeleo chini ya **asilimia 50** na Fungu 14 na Fungu 29 yalikuwa hayajapokea fedha za maendeleo.

#### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

##### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo, ambayo ni pamoja na:-

- (a) Kuendelea kusimamia uwepo wa amani na usalama wa Raia na mali zao;
- (b) Kuendelea kusajili na kutoa vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania, Wakimbizi na Wageni;
- (c) Kuendelea kuzuia na kupeleleza makosa ya jinai na makosa ya usalama barabarani;
- (d) Kuimarisha shughuli za kilimo na mifugo ikiwa ni pamoja na kutekeleza mkakati wa kujitosheleza kwa chakula; na
- (e) Kufanya mapitio ya Sera na Sheria mbalimbali zinazohusu Wizara ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara.; na
- (f) Kuimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopitia majukumu hayo kwa kulinganisha na Bajeti inayoombwa, ilibaini kuwa utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake utaimarika endapo Serikali itatenga fedha za kutosha na kutoa fedha hizo kadri ambavyo

zimeidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara.

#### **4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 407,600,000,000**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la **asilimia 22.9** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambayo yalikuwa **Shilingi 331,591,585,600**. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 28, Fungu 51 na Fungu 93. Ambapo Fungu 28 lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa **asilimia 5**, Fungu 51 lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa **asilimia 120**, Fungu 14 lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa **asilimia 18.9**. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa lengo la makusanyo kwa Fungu 29 limepungua kwa **asilimia 25**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilirejea sababu zilizochangia Wizara kutofikisha lengo la makusanyo kwa Mwaka 2021/2022 na kubaini kuwa elimu ya usalama barabarani, uchakavu wa vitendea kazi, upungufu wa rasilimaliwatu, na upungufu wa vitendea kazi na athari za UVIKO 19 zilikuwa miongoni mwa sababu zilizochangia kupungua kwa makusanyo ya Mafungu hususani Fungu 28, 14 na 93. Pamoja na changamoto hizo bado lengo la makusanyo ya Mafungu hayo limeongezeka kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ni maoni ya Kamati kuwa, pamoja na nia

njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara, ni vema Serikali izingatie changamoto zilizosababisha makusanyo chini ya lengo na ikalenga uhalisia katika kupanga makisio hayo. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa Mafungu yote unaonekana katika **Jedwali Na. 4** hapa chini.

**Jedwali Na. 4: Makadirio ya Mapato**

FUNGU	MAKADIRIO 2021/2022	% YA JUMLA YA LENGO	MAKADIRIO 2022/2023	% YA JUMLA YA LENGO
Fungu 14 - Zimamoto	9,250,000,000	2.79	11,000,000,000	2.69
Fungu 28 - Polisi	90,000,000,000	27.14	94,500,000,000	23.2
Fungu 29 - Magereza	2,000,000,000	0.60	1,500,000,000	0.36
Fungu 51 - Wizara	226,606,000	0.07	500,000,000	0.12
Fungu 93 - Uhamiaji	230,114,979,000	69.4	300,100,000,000	73.6
<b>Jumla</b>	<b>331,591,585,000</b>	<b>100</b>	<b>407,600,000,000</b>	<b>100</b>

**Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo:-

- (a) **Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji** linategemewa kukusanya **asilimia 2.69** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo lilitagemewa kukusanya **asilimia 2.79**, ki-uwiano ikiwa ni pungufu kwa **asilimia 0.10**;
- (b) **Fungu 28 - Jeshi la Polisi** linategemewa kukusanya **asilimia 23.2** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa

na Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo lilitagemewa kukusanya **asilimia 27.14** kiasi ambacho ki-uwiano ni pungufu kwa **asilimia 3.94**;


(c) **Fungu 29 - Jeshi la Magereza** linategemewa kukusanya **asilimia 0.36** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo ilitegemewa kukusanya **asilimia 0.60** ambayo ki-uwiano ni pungufu ya **asilimia 0.24**;

(d) **Fungu 5 1- Wizara** inategemewa kukusanya **asilimia 0.12** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo lilitagemewa kukusanya **asilimia 0.07** ambayo kiuwiano ni ongezeko kwa **asilimia 0.05**; na

(e) **Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji** inategemewa kukusanya **asilimia 73.6** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo ilitegemewa kukusanya **asilimia 69.40** ambayo kiuwiano ni ongezeko kwa **asilimia 4.20**

**Mheshimiwa Spika**, kwa ufafanuzi huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii kama inavyoonekana katika **Grafu Na. 4** ya Taarifa hii. Kamati imebaini kuwa kwa miaka minne mfululizo Mafungu hayo yamekuwa yakikadiriwa na kukusanya asilimia nyingi zaidi ikilinganishwa na Mafungu mengine.

**Grafu Na. 4 : Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo 2021/2022-2022/2023**



*Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022 na 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika makusanyo. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji bado halijapewa uzito unaostahili katika kupelekewa fedha za maendeleo licha ya kuwa ndio inakusanya zaidi ya Mafungu mengine ya Wizara. Hadi mwezi Februari, 2022 Fungu hilo lilikuwa limepokea **asilimia 45.9** tu ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Fungu 93 lipewe uzito unaostahili katika kutengewa na kupelekewa fedha za maendeleo kwa wakati ili kutekeleza miradi yake ya maendeleo kama ilivyoidhinishiwa na Bunge.

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mhesimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa mafungu yote matano ni **Shilingi Trilioni 1.21** Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 600.2** sawa na **asilimia 49.5**, ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 471.2** sawa na **asilimia 39** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 140.4** sawa na **asilimia 11.5** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo zinazombwa, **Shilingi bilioni 133.6** sawa na **asilimia 95.1** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 6.7** sawa na **asilimia 4.9** ni fedha za nje.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho na bajeti kuu ya Serikali na kubaini kuwa wakati Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ni **asilimia 11.5** tu ya Bajeti yote, **asilimia 37.8** ya bajeti kuu imeelekezwa kwenye matumizi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, wakati Bajeti ya Maendeleo ya Bajeti kuu ya Serikali imeongezeka kwa **asilimia 8** ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bajeti ya Wizara iliyotengwa kwa ajili ya Maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 417** ikilinganishwa na Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali itatoa fedha za maendeleo kwa wakati kwa kuzingatia mpangokazi wa miradi husika. Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa



Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni kama inavyoonekana kwenye **Chati Na. 1** hapa chini;

**Chati Na. 1: Mgawanyo wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**



**Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, fedha za nje za maendeleo zilikuwa **asilimia 0.30** ambapo hadi kufikia Februari, 2022 zilikuwa hazijatolewa. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 fedha za maendeleo kutoka nje ni **asilimia 4.7**. Kamati inatoa rai kwa Serikali isitegemee Fedha kutoka nje kwenye miradi ya maendeleo; kwani fedha hizo hazina uhakika wa kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma, Vifungu na Mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na

kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha unaoishia. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

- (a) Bajeti inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imeongezeka kwa **asilimia 28.7** ikilinganishwa na Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko hili lipo katika Mishahara kwa **asilimia 15** na **asilimia 20.25** kwa matumizi mengineyo;
- (b) Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 417** ikilinganishwa na Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (c) Bajeti ya Maendeleo inayoombwa imeongezeka kwa **asilimia 18.9** kwa Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, **asilimia 172** kwa Fungu 29- Jeshi la Magereza, **asilimia 302** kwa Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji; **asilimia 120** kwa Fungu 51- Wizara na kwa Fungu 28- Jeshi la Polisi imeongezeka kwa **asilimia 1525**;
- (d) Fedha za Matumizi Mengineyo zimeongezeka kwa Mafungu yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo: Fungu 14 Jeshi la Zimamoto- imeongezeka kwa **asilimia 24.5**, Fungu 28-Jeshi la Polisi imeongezeka kwa **asilimia 19.7** Fungu 29- Jeshi la Magereza imeongezeka kwa **asilimia 12.3**, Fungu 51- Wizara kwa **asilimia 126**, na Fungu 93- Uhamiaji kwa **asilimia 19.2**.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia na kujadili Randama za Mafungu yote matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi kama nilivyoieleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

- (i) Kukadiria matumizi ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo bila kuzingatia umuhimu wa kufuata taratibu stahiki ili kupata fedha hizo si jambo jema katika utekelezaji bora wa miradi ya Maendeleo.
- (ii) Juhudi kubwa iliyofanywa na serikali katika kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama chini ya Wizara hii ni jambo la kupongezwa. Hata hivyo, upo umuhimu wa kuendelea kufuatilia ipasavyo mtiririko wa fedha kwa ajili ya vyombo hivyo.
- (iii) Kukosekana kwa Hati za Maeneo yanayomilikiwa na majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kutumia maeneo hayo na baadaye kuibuka kwa migogoro ya umiliki.
- (iv) Kutokupatikana kwa Fedha zilizo dhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni jambo linaloathiri tija iliyokusudiwa na mpango wa Mradi.
- (v) Kuhudumia wafungwa wahamiaji haramu **2328** ambao wamemaliza kutumikia vifungo na bado wapo Magerezani inagharimu sh. **2,095,200,000.00** kwa mwaka. Kiasi hicho kinatosha kujenga madarasa 104. Hali hiyo inaonesha umuhimu kwa Serikali kuandaa mkakati wa kuwarejesha

wafungwa hao katika nchi zao ili kuelekeza fedha hizo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini.

## **5.2 Ushauri wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi wa Maoni niliyotoa, ufuatao ni ushauri wa Kamati:-

- (i) Wizara iweke utaratibu wa kufuatilia mtiririko wa fedha za maendeleo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mafungu yake yote matano;
- (ii) Serikali iendelee kuboresha hali ya vyombo vya usafiri na usafirishaji ili kuviwezesha utekelezaji wa majukumu ya majeshi hayo kwa ufanisi zaidi;
- (iii) Uandaliwe mkakati maalum unaotekelezeka wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Majeshi ambayo hayajapimwa; na
- (iv) Serikali izingatie umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kw kufanya hivyo, itasaidia kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo na kupatikana kwa tija ya miradi inayotekelezwa chini ya mafungu yote ya Wizara hii.

## **5.3 Ushauri Mahsus**

### **5.3.1 Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

- (i) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lisimamiwe ili liweze kukamilisha taratibu mbalimbali ikiwemo za ununuzi wa umma. Kwa kufanya hivyo, Fedha fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka Hazina zitaweza kupatikana na kufanikisha miradi hiyo ikiwemo ununuzi wa

magari mawili ya kuzima moto kabla ya Julai, 2022.

- (ii) Uandaliwe mpango mkakati wa mafunzo maalum ikiwemo nje ya nchi ili kuwapata *Divers* kwa idadi inayohitajika. Kwa sasa idadi ya *Divers* katika jeshi hilo hailingani na mahitaji.
- (iii) Uandaliwe utaratibu utakaozitaka Mamlaka za Maji zinapokamilisha ujenzi wa *Fire Hydrants* katika Miji na Majiji zikabidhi kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Lengo ni kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuzifanyia matengenezo pamoja na maboresho mbalimbali. Utaratibu huu utekelezwe sambamba na kuliongezea Jeshi hilo bajeti kwa ajili hiyo.
- (iv) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lijipange kutumia mbinu za kiteknolojia na za kisasa katika kupambana na majanga mbalimbali. Kufanya hivyo, itasaidia jeshi hilo kutoa huduma katika miradi mikubwa ya kimkakati kama vile, upanuzi wa viwanja vya ndege, Reli ya SGR na Bwawa la Mwalimu Nyerere.
- (v) Pamoja na ushauri wa jumla kuhusu masuala ya hati za maeneo ya Majeshi; Wizara ya Mambo ya Nadni ya Nchi iwasiliane na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ili kuiomba Bodi ya TAZARA iridhie na kukikabidhi kiwanja kilichojengwa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dare es Salaam kilichopo Temeke, Mchicha. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lianze mchakato wa

kupata Hati ya kumiliki maeneo ambapo kuna ofisi zake nchini.

### 5.3.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi

- (i) Askari wa Jeshi la Polisi wasimamiwe inavyostahili ili kuzingatia Sheria, taratibu, miiko, weledi na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao.
- (ii) Dhana ya Polisi Jamii itekelezwe kwa ukamilifu katika kupambana na uhalifu hususani katika makazi ya watu;
- (iii) Ili kunusuru taifa lisiendelee kupata hasara itokananyo na kuchakaa kwa Hanga la kuhifadhia Ndege za Jeshi la Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi itoe kibali cha matumizi ya fedha za ukarabati na kuharakisha mchakato wa ununuzi;

### 5.3.3 Fungu 29- Jeshi la Magereza

- (i) Serikali isimamie maandalizi ya mpango mkakati wa muda mrefu na unaotekelezeka wa kuwarejesha katika nchi zao Wafungwa waliomaliza vifungo na bado wapo Magerezani. Bila kufanya hivyo, hali hiyo itaendelea kuchangia msongamano magerezani;
- (ii) Ili kuendelea kushughulikia tatizo la Msongamno magerezani, Serikali iweke utaratibu madhubuti wa kuiwezesha Bodi ya Taifa na Bodi za Mikoa za *Parole* kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria;

- (iii) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya 6 katika mwaka wa fedha 2022/2023, bado kuna umuhimu kwa Serikali kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge. Aidha, upatikanaji wa fedha hizo ulingane na ratiba ya ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa;
- (iv) Jeshi la Magereza liwezeshe kupata magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu ambapo kwa sasa mahitaji halisi ni magari 448;
- (v) Jeshi kuwa na Magereza liandae mkakati wa kuanzisha na kutekeleza kilimo cha mazao ya chakula ikiwemo kilimo cha umwagiliaji. Mkakati huo utaliwezesha jeshi kujitosheleza kwa chakula na kufanya biashara.

#### **5.3.4 Fungu 51- Wizara**

- (i) Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Parole ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kufanya marekebisho.
- (ii) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) iliyokuwa imepanga kununua kadi ghafi kwa ajili ya vitambulisho, iwezeshe kupata kiasi cha shilingi bilioni 5.3 zilizosalia kwa mwaka wa fedha 2021/2022.



- (iii) Pamoja na juhudi za serikali kuanzisha mfumo wa usajili wa Jumuiya kwa njia ya kielektroniki, Serikali ifungue Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kikanda ili kurahisisha huduma kwa wananchi.
- (iv) Pamoja na kupongeza juhudi za Serikali za kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao, Serikali ichukue hatua stahiki na madhubuti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufanikisha zoezo la kuwarejesha wakimbizi hao nchini kwao.
- (v) Serikali iongeze jitihada za kuwafikia kwa urahisi watu wote wenye vigezo vya kusajiliwa na kutambuliwa wanaoishi mbali na makao makuu ya Wilaya.
- (vi) Pamoja na nia njema ya Serikali kutekeleza mpango wa ujenzi wa nyumba za wahanga wa biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ifanye upembuzi wa kina kabla ya kuanza utekelezaji.

#### **5.3.5 Fungu 93 - Uhamiaji**

- (i) Serikali iandae mpango mkakati unaotekelezeka wa kukabiliana na kumaliza kabisa wimbi la wahamiaji haramu kutoka nchi mbalimbali hapa nchini. mkakati huo uende sambamba na kutenga bajeti ya

kuwarejesha wafungwa wahamiaji haramu waliomaliza kutumikia vifungo vyao.

- (ii) Serikali iiwezeshe Uhamiaji kwa vitendea kazi ikiwemo Magari na Pikipiki kwa ajili ya kufanya misako na doria maeneo ya mipakani. Aidha, Uhamiaji wawezeshwe kupata Boti kwa ajili ya kufanya Misako na Doria katika mwambao wa bahari ya Hindi ambayo imekuwa ni njia kubwa ya kupitisha wahamiaji haramu na Magendo.
- (iii) Serikali ichukue juhudi za makusudi za kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katika mipaka yetu pamoja na mwambao wa Bahari ya Hindi. Kufanya hivyo ni sehemu ya jitihada za muda mrefu za kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu nchini.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*):-

1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb	-	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb	-	Mjumbe
4. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb	-	Mjumbe
5. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb	-	Mjumbe
6. Mhe. Janeth Mauris Masaburi, Mb	-	Mjumbe
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb	-	Mjumbe
8. Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb	-	Mjumbe
9. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb	-	Mjumbe
10. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb	-	Mjumbe
11. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb	-	Mjumbe
12. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb	-	Mjumbe
13. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb	-	Mjumbe
14. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb	-	Mjumbe
15. Mhe. Muharami Shaban Mkenge, Mb	-	Mjumbe
16. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb	-	Mjumbe
17. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb	-	Mjumbe
18. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb	-	Mjumbe
19. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb	-	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Eng. Hamadi Yusuf Masauni (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb), Katibu Mkuu

Ndugu Christopher Kadio, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ramadhan Kailima pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nanelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.



Vita Rashidi Kawawa, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO  
YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

05 Mei, 2022

**UTELEKEZAJI WA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA (NUU) KATIKA MPANGO NA  
BAJETI YA MWAKA 2021/2022**

---

**1.0 FUNGU 14 – JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**1.1 Ushauri wa Jumla**

***1.1.1 Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa Watumishi katika Idara na Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutokana na Umuhimu wake katika usalama wa Raia na Mali zao.***

Agizo limezingatiwa. Katika mwaka 2021/22 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeajiri Askari 400 ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

***1.1.2 Serikali ione umuhimu wa kuwa na Mpango Mkakati wa kujenga nyumba za makazi kwa ajili ya Watumishi na Askari wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hii itaondoa changamoto ya muda mrefu ya makazi kwa askari ambao wengi wao wanakaa uraiani jambo ambalo si zuri kiusalama.***

Agizo limezingatiwa. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea na ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya familia za Askari 80 katika eneo la Kikombo Jijini Dodoma. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa miaka

10 wa ujenzi wa ofisi, vituo na makazi ya maafisa na askari utakaoanza kutekelezwa mwaka 2022/23.

**1.1.3 Serikali iyawezeshe Majeshi yake kwa kuyapatia vyombo vya usafiri na usafirishaji ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi**

Agizo limezingatiwa. Katika mwaka 2021/22 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekamilisha ununuzi wa magari 25 kwa ajili ya shughuli za utawala na ukaguzi. Aidha, katika mwaka 2022/23, Jeshi limepanga kununua magari mengine mapya 19 kwa ajili ya shughuli za utawala na ukaguzi.

**1.1.4 Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo yanaendelea kukua kutokana na kutokulipwa kwa stahiki mbalimbali za Wastaafu, Watumishi na madeni ya wazabuni na watoa huduma. Aidha, Serikali kupitia Hazina ilipe madeni yote yaliyohakikiwa, kipaumbele kitolewe kwa Wastaafu.**

Agizo limezingatiwa. Katika mwaka 2021/22 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea **Shilingi 27,451,176.22** kwa ajili ya madeni ya Wazabuni. Aidha, uhakiki wa madeni mengine yenye jumla ya **Shilingi 1,680,529,719.46** umefanywa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kwa ajili ya taratibu za malipo

**1.1.5 Serikali itenge na kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kwa Mafungu yote ya Wizara ili kutekeleza kwa ufanisi miradi inayopangwa.**

Katika mwaka 2021/22 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetengewa fedha **Shilingi bilioni 3.5** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, taratibu za ununuzi zinaendelea kukamilishwa ili kupatiwa fedha hizo kutoka Wizara ya fedha na Mipango

## 1.2 Ushauri Mahsus

### ***1.2.1 Serikali itenge fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo la kituo cha uokoaji na litumike kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji katika Mkoa wa Dar es Salaam.***

Agizo limezingatiwa. Serikali imeshatoa fedha **Shilingi 2,397,178,675.40** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la zimamoto na uokoaji lililopo TAZARA (Mchicha), Dar es Salaam na ujenzi upo katika hatua za umaliziaji. Hadi kufikia tarehe 12 Machi, 2022 kiasi cha **Shilingi 2,134,141,626.15** kilikuwa kimetumika.

### ***1.2.2 Serikali iongeze ukomo wa bajeti ya maendeleo ya Jeshi la Zimamoto na kutoa fedha hizo kwa ukamilifu kuendana na mahitaji halisi ya Jeshi.***

Katika mwaka wa fedha 2021/22 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetengewa fedha Shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na katika mwaka 2022/23 Jeshi litatengewa fedha za maendeleo **Shilingi bilioni 9.93**. Aidha, Serikali itajitahidi kuongeza ukomo wa bajeti ya maendeleo kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kila mwaka kadri hali itakavyoruhusu.

**1.2.3 Serikali itoe kipaumbele katika kuajiri askari wa kutosha kulingana na miradi ya kimkakati inayoendelea ambayo itahitaji huduma za zimamoto na uokoaji. Miradi hiyo ni pamoja na ile ya upanuzi wa viwanja vya ndege, miradi ya umeme na gesi na ujenzi wa bomba la mafuta.**

Agizo limezingatiwa. Katika mwaka 2021/22 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeajiri Askari 400 ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Serikali itaendelea kulipatia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji vibali vya ajira mpya kadri bajeti itakavyoruhusu.

**1.2.4 Wizara iangalie upya tozo zilizopangwa kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa vya zimamoto ambapo gharama yake ni kubwa kulingana na hali halisi ya vipato vya wananchi, jambo linalochangia wananchi wengi kushindwa kulipa na hivyo Serikali kupoteza mapato yatokanayo na tozo hizo.**

Agizo limezingatiwa. Kanuni ya tozo imeshafanyiwa marekebisho na zimewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua zaidi.

## **2.0 FUNGU 28 – JESHI LA POLISI**

**2.1 Kamati ilishauri Serikali kuyawezesha majeshi yake kwa kuyapatia vyombo vya usafiri na usafirishaji ili kuweza kutekekeza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.**

Serikali inaendelea kuliwezesha Jeshi la Polisi kwa kulipatia vyombo vya Usafiri. kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 serikali ilitoa kiasi cha Shilingi Bilioni 5.7 kwa ajili ya ununuzi



wa Magari ya Misafara ya Viongozi wakuu wa Serikali na Viongozi wakuu Waandamizi wa Jeshi la Polisi. Jumla ya Magari 25 yamenunuliwa kupitia Wakala wa Ununuzi na Ugavi wa Serikali (GPSA) T/L/Cruiser VXR 1, T/L/Cruiser Prado 17, T/L/Hilux 7 na Bajaji 1.

Pia tunategemea kupokea Magari 369 katika Mkataba wa Magari 777 ME.014/PF/2012/2013/G/40 between Ministry of Home Affairs, Tanzania and Ashok Leyland LTD, India.

**2.2 Kamati ilishauri Serikali itoe fedha za maendeleo kwa miradi ya muda mrefu iliyokuwa imeidhinishiwa fedha katika mwaka wa fedha 2020/2021. Hii ni pamoja na mradi wa kukamilisha kituo cha Polisi cha Mkokotoni ambapo ujenzi wake umesimama tangu mwaka 2013 licha ya kuwa mradi huo ulikwisha tekelezwa kwa asilimia 60.**

Katika kutekeleza Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetoa fedha shilingi 1,850,000,000 ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyokuiwa imeidhinishwa. Aidha katika kukamilisha ujenzi wa kituo cha Polisi Mkokotoni, kiasi cha shilingi 352,106,750 zimeishatolewa kwa ajili ya kukamalisha kituo hicho.

**2.3 Ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia, Kamati iliishauri Serikali kutenga Bajeti ya Kutosha na kutoa fedha hizo kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi kukabiliana na makosa mbalimbali yakiwemo makosa ya Kimtandao (Cybercrime) na makosa yanayovuka mipaka (Transnational Crime). Aidha, kitengo cha uchunguzi**

***(Forensic Bureau) kiwezeshe kutekeleza majukumu yake kwa Ufanisi.***

Serikali imepokea ushauri wa kamati na Jeshi la Polisi liliomba na kupewa kifungu (subvote) namba 7004 inayotumiwa na Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi. Hivyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga katika kifungu hicho cha 7004 kiasi cha shilingi 404,120,000 ili kuiwezesha Kamisheni hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama ilivyoshauriwa na kamati.

***2.4 Kamati ilishauri Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa deni la Jeshi la Polisi linalohusu Watumishi, Wastaafu, madeni ya wazabuni na watoa huduma ambayo yanaendelea kukua kutokana na kutolipwa kwa stahiki mbalimbali. Aidha Serikali kupitia Hazina ilipe madeni yote yaliyohakikiwa, kipaumbele kitolewe kwa wastaafu.***

Jeshi la Polisi tunayo madeni yaliyo hakikiwa na kukubaliwa yenye jumla ya shilingi 366,182,669,419.41 ikiwa shilingi 34,479,476,752.07 ni madeni ya watumishi, shilingi 311,693,273,065.86 ni madeni ya wazabuni na shilingi 20,009,919,601.48 ni madeni ya watoa huduma. Madeni mengine yaliyobaki ya mehakikiwa katika ukaguzi ulioanza tarehe 07.02.2022 na kumalizika tarehe 06.03.2022, matokeo yaripti ya uhakiki huo haijakamilika.

Kwa kipindi cha kuanzia 01 Julai 2021 hadi kufikia tarehe 08 Machi, 2022, tumepokea kiasi cha shilingi 52,421,284,340.44 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyoha kikiwa na kukubaliwa na shilingi 2,075,730,790.25 kwa ajili ya kulipa mizigo na nauli za wastaafu. Kwa msingi huo ulipaji wa madeni katika kipindi tajwa umefikia jumla ya shilingi 54,497,015,130.67.

**2.5 Kamati ilishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa watumishi kwa Jeshi la Polisi kutokana na umuhimu wake katika usalama wa Raia ma mali zao.**

Jeshi la Polisi linaishukuru Serikali kupitia Kamati ya Bunge Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama (NUU) kwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2021/2022 Jeshi la Polisi limefanikiwa:-

- (a) Kupata kibali cha Ajira Mbadala (permit) ya watumishi **3,103** kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao kwa sasa wapo Shule ya Polisi-Moshi (TPS) kwa ajili ya kuhudhuria mafunzo ya awali ya Jeshi la Polisi.
- (b) Kupata kibali cha Ajira Mpya ya watumishi **1,000** kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao kwa sasa wanaendelea na mafunzo ya awali ya Jeshi la Polisi katika Shule ya Polisi-Moshi (TPS).

Mara baada ya kuhitimu mafunzo hayo ya awali ya Jeshi la Polisi jumla ya Askari **4,103** watasaidia kudumisha usalama wa Raia na Mali zao.

**2.6 Kamati ilishauri Serikali ione umuhimu wa kuwa na mpango mkakati wa kujenga nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi na Askari wa Jeshi la Polisi. Hii itaondoa changamoto ya muda mrefu ya makazi kwa askari ambao wengi wao wanaishi uraiani jambo ambalo si zuri kiusalama.**

Serikali kupitia Mpango wa tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka mitano *Five Years National Development Plan 2021/2022- 2025/2026*, imepanga kulijengea Jeshi la Polisi Jumla ya nyumba 2000 na vituo vya Polisi 35 Nchi nzima ifikapo June, 2026 kwa thamani ya **Shilingi 160,000,000,000.00**. Sambamba na hilo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeandaa Mpango Mkakati wa kujenga Jumla ya nyumba 6933 kwa ajili ya Watumishi na Askari wa Majeshi yaliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha miaka kumi 2021/2022 hadi 2031/2032. Aidha, Jeshi la Polisi kupitia Mpango Mkakati wa Jeshi la Polisi 2020/2021 hadi 2025/2026 umepanga kujenga jumla ya nyumba 2500 ifikapo June, 2026.

Ni imani ya Jeshi la Polisi kuwa endapo Serikali itatekeleza mipango hii, italisaidia Jeshi la Polisi kupunguza changamoto hii kubwa ya makazi kwa askari wake.

***2.7 Kamati inaendelea kuishauri Serikali iongeze na kuendeleza juhudi za kufanikisha utekelezaji wa miradi ya Maendeleo inayowasilishwa Bungeni na fedha zake kuidhinishwa na Bunge. Kufanya hivyo, kutaliwezesha Bunge kuongeza tija katika ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za umma inavyostahili.***

Jeshi la Polisi linaishukuru Kamati kwa msukumo na kuendelea kuishauri serikali iongeze fedha na juhudi za kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyo idhinishwa na Bunge la Bajeti. Msukumo huo umeliwezesha Jeshi la Polisi kutengewa **Shilingi 2,000,000,000.00** za Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo mpaka kufikia mwezi December, 2021 Kiasi cha **Shilingi 1,850,000,000** sawa na **asilimia 98** zimetolewa.

**2.8 Kamati inaishauri Serikali kushughulikia changamoto za kimkataba zilizojitokeza katika mradi wa ujenzi wa nyumba 353 za Maafisa, Wakaguzi na Askari wa vyeo mbalimbali kwa ubia na mwekezaji wa sekta binafsi katika eneo la Msasani namba 29 Kunduchi jijini Dar es Salaam ambapo nyumba hizo zimeanza kutumika.**

Changamoto za kimkataba zilizojitokeza zimeshughulikiwa na Timu maalum ya Serikali iliyopitia mkataba kwa kushirikiana na Mwekezaji ili kupata suluhu ya pamoja katika maeneo mbalimbali yaliyojitokeza. Kupitia hatua hiyo Serikali iliweza kuzipokea nyumba 353 za askari na maafisa na tayari kuanza matumizi ya kambi ya kunduchi na Mikocheni pamoja na kituo cha Polisi Oysterbay. Vilevile, mwekezaji ameendelea kutoa ushirikiano wa marekebisho ya mapungufu ya kiujenzi pale panapojitokeza uhitaji.

Serikali inachukua fursa hii kupongeza jitihada za kamati ya Bunge kusaidia mafanikio ya hatua hii muhimu ya kupunguza changamoto za makazi kwa askari. Kwa upande wa utekelezaji wa mradi huu, mwekezaji ameomba muda wa kujadiliana na wabia wake (wenye hisa na wawezeshaji) ili kutathimini nia na uwezo wa kuendelea na uwekezaji wa mradi huo.

### **3.0 FUNGU 29 – JESHI LA MAGEREZA**

**3.1 Kamati inampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kutoa Msamaha wa Wafungwa 5000 katika Sikukuu ya Muungano tarehe 26 Aprili, 2021. Msamaha uliotolewa kwa Wafungwa umeipunguzia Serikali gharama ya takribani Shilingi 4,075,000 kwa siku ambapo**

***kwa Mwaka ni shilingi 1,487,375,000. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zote zitakazoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka 2021/2022 kwa ajili ya vikao vya Bodi ya Taifa na za Mikoa za Parole ili wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa msamaha wapunguzwe magerezani na hatimaye kuokoa fedha za Serikali zinazotumika kuwatunza ambapo kwa sasa takribani Shilingi 26,363,620 hutumika kwa siku sawa na Shilingi 9,622,721,300 kwa Mwaka;***

Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Fungu 29: Jeshi la Magereza limepokea fedha ya vikao vya Bodi ya Parole kiasi cha Shilingi.58,765,300.00 kwa ajili ya vikao vya Parole. Kutofanyika kwa vikao vya Parole kwa kiasi kikubwa kulichangiwa na kuisha muda wa Bodi ya Parole iliyokuwepo. Sababu kubwa ya mpango wa Parole kutonufaisha wafungwa wengi inahusiana na mfumo wa kisheria na taratibu za kumtoa mfungwa kwa mpango huo.

Makundi ya wafungwa wasionufaika na mpango wa Parole ni wale waliohukumiwa kwa makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha, madawa ya kulevya, na makosa yanayohusiana na kujamiiiana. Wengine ni wafungwa waliohukumiwa kifungo cha maisha, waliobadilishiwa adhabu kutoka hukumu ya kifo na wale ambao hawajatimiza vigezo vya miaka minne gerezani au theluthi moja ya kifungo, hata kama makosa yao zinakidhi vigezo vya kisheru kutolewa kwa mpango wa Parole. Pamoja na kutimiza masharti, ili mfungwa atolewe kwa mpango wa Parole, lazima jamii waliotendewa ubaya/uvunjifu wa sheria wakubali mfungwa huyo kutolewa.

**3.2 Pamoja na jitihada za Serikali katika kujenga Magereza mapya ili kutatua tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani, bado Jeshi la Magereza linakabiliwa na changamoto hiyo ambapo uwezo wa magereza yaliyopo ni kuhifadhi wahalifu 29,902 kisheria kwa siku ikilinganishwa na wastani wa wahalifu 32,348 waliopo kwa siku katika kipindi hiki. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya. Kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya Shilingi 840,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Magereza Makuu na hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya.**

Katika jitihada za kupunguza msongamano, Jeshi la Magereza limeanza kujenga magereza ya wilaya za Kilosa na Karatu. Gereza Kilosa limeanza kujengwa kwa kutumia fedha ya fidia iliyotolewa baada ya gereza la awali kuondolewa kupisha ujenzi wa reli ya treni ya umeme na Gereza Karatu limeanza kujengwa kwa kutumia vyanzo vya ndani ya Jeshi. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi. 4,569,600,000.00 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa magereza hayo mawili na kuanza ujenzi wa magereza mengine manne ambayo ni Kakonko, Kaliua, Gairo na Msalato.

**3.3 Serikali iliwezeshe Jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu ambapo kwa sasa mahitaji halisi ni magari 480. Upatikanaji wa magari hayo, pamoja na mambo mengine, utasaidia mahabusu kupata nafasi ya kusikiliza kesi zao kwa wakati**

***uliopangwa na hivyo kuamuliwa mapema. Hii itapunguza msongamano wa wafungwa na Mahabusu Magerezani lakini pia itaondoa changamoto ya mahabusu kukaa muda mrefu magerezani bila kesi zao kuamuliwa;***

Serikali kupitia bajeti ya Jeshi la Magereza yam waka 2022/23 imetenga kiasi cha shilingi 5.7 bilioni kwa ajili ya kununua magari ya utawala na mabasi ya kusafirishia mahabusu. Mabasi hayo yatasaidia kupunguza changamoto ya matumizi ya mabasi yaliyochakaa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Dodoma na Arusha. Aidha, Serikali kupitia Jeshi la Magereza itaendelea kutenga fedha ya kununua magari ya mahabusu kila mwaka kwa lengo la kuondoa kabisa tatizo la usafiri kwa mahabusu.

Vilevile, kwa kushirikiana na Idara ya Mahakama, huduma ya kuendesha kesi kwa kutumia luninga (video conferencing) inafanyika katika baadhi ya magereza hapa nchini. Utaratibu huu unafanyika ili kupunguza gharama za kusafirisha wafungwa na mahabusu kwenda kusikiliza kesi. Pia vikao vya kamati za kusukuma mashauri (case flow management committee) vinafanyika na kupitia kesi zote zilizokaa muda mrefu bila kusikilizwa.

***3.4 Tangu Mwaka 2016 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali na jiko katika Gereza la Segerea. Hata hivyo ushauri huo haujawahi kuzingatiwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha hizo ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo ambayo ni muhimu kwa Gereza la Segerea;***



Serikali kupitia Jeshi la Magereza imetenga Shilingi. 50,000,000.00 katika bajeti ya mwaka 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi wa jiko la Gereza Segerea. Aidha, Jeshi la Magereza linaendelea na ujenzi wa Hospitali Kuu ya Magereza eneo la Ukonga, Dar es Salaam ambayo itatumika kwa rufaa ya maafisa, askari na wafungwa kutoka mikoani wanaokuja kutibiwa jijini Dar es Salaam. Kwa kuwa hospitali ya Segerea ilikusudiwa kwa ajili ya rufaa ya wafungwa, hitaji hilo limezingatiwa katika ujenzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi iliyoko Ukonga.

**3.5 Serikali itoe fedha kwa ajili ya kuwezesha vikao vya Bodi ya Taifa na Bodi za Mikoa za Parole. Kuwezesha vikao vya Bodi hizi kutasaidia wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa parole kupunguzwa magerezani.**

Jeshi la Magereza kwa kuona umuhimu wa mpango wa Parole limetenga Kifungu kinachojitegemea kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Parole tu. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga jumla ya Shilingi.139,100,000.00 kwa ajili ya shughuli za Parole. Kwa muda mrefu Bodi ya Parole ilikuwa imemaliza muda wake na hivyo hapakuwa na vikao vya Bodi ya Parole ya Taifa, kwa kuwa Bodi imeshateuliwa Jeshi la Magereza katika mwaka 2022/2023 limeongeza bajeti ya Parole na kufikia Shilingi 324,688,000.00 kutoka shilingi 139,100,000 zilizotengwa mwaka uliopita ili kuwezesha shughuli za Parole vikiwemo vikao vinne vya Bodi za Taifa na Mikoa kufanyika kwa ufanisi kwa mwaka.

**3.6 Serikali itoe jumla ya shilingi milioni 840 zilizotengwa katika Mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati mabweni na miundombinu ya Magereza 12 nchini. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa;**

Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi 840,000,000.00 katika bajeti ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya ukarabati wa magereza. Fedha hiyo imeshatolewa na taratibu za kuipokea kutoka hazina zinaendelea. Ukarabati wa miundombinu ya magereza utanza mara tu fedha zitakapopokelewa.

**3.7 Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa Shilingi 3,615,000,000.00 zilizotengwa katika mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mpunga la Gereza la Idete na ununuzi wa zana za kilimo. Aidha, kwa Mwaka 2021/2022 Serikali imetenga Shilingi Bil 6 kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za mazao mbalimbali na kununua zana za kilimo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. Pamoja na juhudi hizo za Serikali, Kamati inashauri Jeshi kuwa na mpango mkakati wa kuanzisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Magereza mengine ili Jeshi hilo liweze kujitoshleza kwa chakula na kuzalisha kwa ajili ya biashara.**

Katika mwaka wa fedha 2021/22 Jeshi la Magereza limeendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Gereza Idete. Kwa sasa ujenzi wa mfereji mkuu wa kutoa maji mtoni kuyapeleka shambani umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2022/23 Shilingi 2,800,000,000.00

zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji shambani ili uzalishaji uanze. Aidha Jeshi la Magereza linao mpango mkakati wa kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika magereza mbalimbali ambapo kwa mwaka 2022/2023 Shilingi 2,500,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuongeza miundombinu mingine ya umwagiliaji katika magereza matatu ya Kalilankulukulu, Kitete na Ushora.

#### 4.0 FUNGU 51 - WIZARA

**4.1 *Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa kiasi cha Shilingi 6,319,692,308 kwa ajili ya Mradi wa Vitambulisho vya Taifa ikiwemo kununua kadi ghafi kwa ajili ya vitambulisho. Hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri Serikali kuwa ihakikishe inazalisha vitambulisho vyote kulingana na idadi ya namba za utambulisho ambazo zimekwisha tolewa kwa wananchi ifikapo Mwezi Juni, 2021 kama ilivyokuwa imepangwa.***

Ushauri wa Kamati umepokelewa, Mamlaka inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza kasi ya uzalishaji na ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa ili kuhakikisha watu wote wenye namba za utambulisho wanapatiwa vitambulisho. Mkakati wa Mamlaka ilikuwa ni kuzalisha vitambulisho kwa maombi yaliyo tayari hadi kufikia mwezi Juni, 2021.

Hata hivyo, mkakati huo, haukutekelezwa kikamilifu kutokana na kutopatikana kwa kadi ghafi za uzao wa pili kwa wakati kwa ajili ya kuzalisha vitambulisho vya Taifa, hivyo kupelekea kuwepo kwa marejeo ya mpango kazi uliokuwepo hapo awali kwa kuzingatia hali halisi. Hadi

kufikia Februari, 2022 Mamlaka imezalisha vitambulisho 10,752,333 na vitambulisho 9,982,281 vimesambazwa na kugawiwa kwa wananchi. Aidha, Mpango wa Mamlaka ni kuzalisha vitambulisho kwa watu wenye namba za utambulisho kufikia Desemba, 2022.

**4.2 Serikali iongeze jitihada za kuwafikia kwa urahisi watu wote wenye vigezo vya kusajiliwa na kutambuliwa wanaoishi mbali na makao makuu ya wilaya. Hii ni pamoja na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari ili kuwezesha wataalamu kuwafikia walengwa wengi zaidi.**

Ushauri umezingatiwa. Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inaendelea kufanya usajili na utambuzi wa wananchi wenye vigezo katika ofisi za usajili za wilaya 151 nchini. Aidha, ili kuwafikia kwa urahisi watu wengi wenye vigezo vya kusajiliwa na kutambuliwa wanaoishi katika maeneo ya vijijini, Mamlaka imekuwa ikifanya usajili wa mkupuo (mass registration) katika ngazi za vijiji, mitaa na shehia. Usajili huo hufanyika kulingana na uhitaji wa usajili katika maeneo husika ambapo watu wengi wameendelea kusajiliwa na kutambuliwa.

Mamlaka pia imefungua vituo vya usajili nje ya makao makuu ya wilaya katika baadhi ya wilaya kwa kuzingatia jiografia ya maeneo, miundombinu na idadi ya watu katika wilaya. Lengo ni kuhakikisha watu wote wenye vigezo wanafikiwa na kupatiwa huduma ya usajili na utambuzi. Vituo hivyo ni pamoja na Kituo cha Utambuzi na Usajili cha Morogoro Vijijini ambacho kinaendelea kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, katika matukio mbalimbali ya kitaifa, Mamlaka pia imekuwa ikiendesha zoezi la usajili na utambuzi wa wananchi.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu, Serikali imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali ikiwemo vifaa vya TEHAMA na magari. Katika mwaka 2020/2021 Mamlaka imefanikiwa kununua magari matano (5), mwaka 2021/2022 inatarajia kununua magari manne (4) pamoja na vitendea kazi vingine ikiwemo vifaa vya TEHAMA, na pia katika mwaka 2022/2023 yatanunuliwa magari sita (6). Aidha, Mamlaka imeendelea kushirikiana na Halmashauri na Taasisi mbalimbali za Serikali zilizopo wilayani kwa ajili ya kupatiwa magari ili kutekeleza shughuli za usajili na utambuzi zinaoendelea katika wilaya husika.

**4.3 Mikataba ya Manunuzi ya Mitambo ya uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa ijumuishe mafunzo ya muda mrefu kwa Wataalamu wa ndani bila ya gharama ya ziada ili kuwezesha Serikali kumiliki, kuendesha, kuhudumia na kukarabati mitambo hiyo jambo ambalo litaepusha gharama kubwa zinazotumika kwa kutegemea wataalamu kutoka nje.**

Ushauri umepokelewa na kuzingatiwa. Aidha, mkataba wa mashine mpya za uzalishaji vitambulisho ulijumuisha mafunzo ya matumizi ya mashine pamoja na kufanya matengenezo madogo. Watumishi sita (6) walipata mafunzo kwa ajili ya kutumia mashine na kufanya ukarabati kwa muda wa siku kumi (10) nchini Ujerumani na Ufaransa. Aidha, baada ya mashine kufungwa watumishi 25 walipatiwa mafunzo kuhusu utumiaji wa mashine hizo kwa muda wa siku 14. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani wa

Mamlaka ili kupunguza utegemezi wa wataalamu wa nje ya nchi.

Vilevile, katika mwaka wa fedha 2021/22, Mamlaka inatarajia kutoa mafunzo zaidi kwa wataalamu wake hususan mafunzo saidizi na matengenezo (*support and maintenance*) kwa kuwa mkataba wa ununuzi wa mashine unatoa fursa ya mafunzo. Mafunzo hayo yatatolewa na mtaalam ambaye ameteuliwa na mkandarasi na yatatolewa kwa watumishi wa Mamlaka ili kuwajengea uwezo zaidi na kupunguza utegemezi kwa wakandarasi.

**4.4 *Serikali ikamilishe mfumo wa kielektroniki wa Usajili wa Jumuiya ili kuwezesha malipo ya kielektroniki kupatikana mahali popote nchini. Hii, pamoja na mambo mengine, itaongeza mapato ya makusanyo yatokanayo na Usajili wa Jumuiya.***

Wizara kupitia ofisi ya Msajili wa Jumuiya imekamilisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Jumuiya (*Registration of Society Management Information System – RSMIS*). Kwa sasa mfumo huu uko kwenye hatua ya majaribio, ambapo majaribio hayo yanahusisha matumizi ya ndani kabla ya kuanza kutumiwa na wateja wa nje. Lengo ni kuhakikisha kuwa mfumo huu unaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2022/23.

## 5.0 FUNGU 93 – JESHI LA UHAMIAJI

### 5.1 Kamati inashauri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa watumishi katika Idara na majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

*Mheshimiwa Mwenyekiti*, Kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepata kibali cha Kuajiri Askari Konstebo wapya wa Uhamiaji katika awamu mbili. Awamu ya kwanza, kilitolewa kibali cha kuajiri Askari wapya **350** na awamu ya pili nafasi **470**, kwa ujumla kufanya kibali cha nafasi **820**.

*Mheshimiwa Mwenyekiti*, Tayari Askari wapya **820** utaratibu wa awali wa ajira umekamilika, wameshapokelewa na mafunzo yameshafunguliwa katika Kambi ya Mafunzo ya Uhamiaji kwa Kozi Na. 01/2022 huko Boma Kichakamiba Wilayani Mkinga katika Mkoa wa Tanga.

### 5.2 *Serikali ione umuhimu wa kuwa na Mpango Mkakati wa kujenga nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi na Askari wa majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;*

*Mheshimiwa Mwenyekiti*, kwa kutambua changamoto hii, Wizara imeandaa Mpango Kabambe wa ujenzi wa nyumba, ofisi na vituo kwa ajili ya vyombo vya Ulinzi na Usalama. Mpango huu umekamilika katika ngazi ya wataalamu na kuwasilishwa Wizarani ili kupata muongozo kwa ajili ya kuendelea na hatua za utekelezaji.

**5.3 Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi katika majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya watumishi, watoa huduma na wazabuni. Aidha, Serikali kupitia Hazina ilipe madai yote yaliyohakikiwa hasa ya wastaafu.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Madeni ya Jeshi la Uhamiaji yaliyoishia mwezi Juni, 2021 yenye jumla ya **Shilingi 3,326,013,773.34** yalihakikiwa na Timu kutoka HAZINA. Mchanganuo wa Madeni yaliyohakikiwa ni kama ifuatavyo; watumishi ni Shilingi **2,527,789,152.00**; wazabuni ni **Shilingi 750,229,928.32**; Wakandarasi ni Shilingi **18,923,089**; Watoa Huduma ni **Shilingi 26,371,604.02** na mengineyo ni **Shilingi 2,700,000.00**.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, baada ya zoezi la uhakiki, deni lililokubaliwa ni Shilingi **2,716,668,696.36** kwa mchanganuo ufuatao; Shilingi **2,308,695,860.00** ni madeni ya watumishi; Shilingi **366,589,821.34** ni madeni ya Wazabuni; Shilingi **15,975,600.00** ni madeni ya Wakandarasi na Shilingi **25,407,415.02** ni madeni ya Watoa huduma. Baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa madeni haya, hatua inayofuata sasa Serikali kupitia Bajeti yake inatarajia kulipa madeni haya.

**5.4 Uhaba wa vyombo vya Usafiri vitakavyowezesha Jeshi la Uhamiaji kukabiliana na majukumu yake ya kila siku ikiwemo doria, kuwabaini wahamiaji haramu na ukusanyaji wa Intalijensia;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa vyombo vyo usafiri ndani ya Jeshi la Uhamiaji. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Jeshi la Uhamiaji imenunua jumla ya magari 6 na katika mwaka wa fedha 2022/2023 Idara imepanga kununua jumla ya



magari 30 kwa ajili ya doria na misako ya wahamiaji haramu.

- 5.5 Fedha za Miradi ya Maendeleo hazitolewi kwa wakati na kwa mtiririko unaotakiwa. Kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 fedha zilizotengwa zilikuwa Shilingi 4,450,000,000.00 lakini hadi kufikia mwezi Februari 2021 fedha zilizopokelewa ni Shilingi 400,000,000.00 tu sawa na asilimia 8.99;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mawasiliano kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Fedha na Mipango yameendelea kufanyika kuhusu kuipatia Fedha Miradi ya ujenzi inayotekelezwa ndani ya Jeshi la Uhamiaji. Mwaka wa fedha 2021/2022 Jeshi la Uhamiaji ilitengewa Shilingi **4,050,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Idara imekwishapokea kiasi cha Shilingi **1,859,825,087.36** ambayo ni sawa na asilimia **45.92** ya bajeti ya mwaka.

- 5.6 Jeshi la Uhamiaji ipewe Stahiki zake zote kama ilivyoainishwa katika Muundo wake;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Baada ya Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 rejeo la Mwaka 2016 kufanyiwa marekebisho, Jeshi la Uhamiaji imeshatambuliwa kuwa Jeshi kamili na kupata stahiki zote na tayari Kanuni kwa ajili ya Haki na Stahili zimeandaliwa na zipo tayari kwa utekelezaji.

- 5.7 Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 rejeo la Mwaka 2016 ifanyiwe marekebisho ili Idara hiyo itambulike rasmi kama Jeshi;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Jeshi la Uhamiaji ilitambulika rasmi kuwa Jeshi kupitia mabadiliko ya Sheria mbalimbali Na. 5 ya mwaka 2021 katika Bunge la 11 Mkutano wa 4

Kikao cha 6, ambapo Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 rejeo la Mwaka 2016 ilifanyiwa marekebisho.